# CLASS 8 END TERM 2 2020

# KISWAHILI

MUDA: Saa 1 dakika 40

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.***

Ubongo wa mwanadaumu___1___hai hufanya kazi kila wakati awe macho au amelala. Utendaji kazi ___2___huendeshwa na glukosi mwilini. Kwa hivyo vyakula___3___sukari hii ni muhimu kuliwa.___4___, lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili una kiwango cha sukari___5___maisha. Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda. Njia ya pili ya kukumbuka mambo ni___6___ vileo kama pombe na nikotini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.___7___ mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni muhimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa na kuhusisha jina na kile___8___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. mwenye | B. alio | C. aliye | D. mwenye aliye |
| 2. | A. wake | B. yake | C. zake | D. lake |
| 3. | A. zenye | B. vyenye | C. chenyewe | D. vyenyewe |
| 4. | A. Kwa hivyo | B. Kwa vile | C. Hata vile | D. Hata hivyo |
| 5. | A. kinachorekebisha | B. kisichohatarisha | C. kitakachosawazisha | D. kisichopunguza |
| 6. | A. kupiga hatua | B. kupiga msasa | C. kupiga marufuku | D. kupiga ubwete |
| 7. | A. Huenda | B. Endapo | C. Lakini | D. Ila |
| 8. | A. linalolengwa | B. zinazolengwa | C. litakalolengwa | D. kinacholengwa |

Ulikuwa ni wakati wa macheo na___9___ulikuwa ungalipo. Kila mmoja wetu alionekana___10___kutekeleza ___11___wa siku hiyo. Hata wanawake___12___nyuma. Ukumbi wa mikutano ulikuwa umepambwa na kunakishiwa vilivyo, hivyo basi ulionekana maridadi kabisa. Mwendo wa___13___yaani mchana, shere ilianza___14___kwani wageni walioalikwa walionekana___15___katika ukumbi wa sherehe.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. ukungu | B. umande | C. uwingu | D. weusi |
| 10. | A. akienda nguu | B. akilia ngoa | C. akivunja mgongo | D. akiona hasara |
| 11. | A. jukumu | B. wajibu | C. wadhifa | D. mambo |
| 12. | A. wangeachwa | B. wataachwa | C. waliachwa | D. hawakuachwa |
| 13. | A. alasiri | B. adhuhuri | C. macheo | D. machao |
| 14. | A. kusonga | B. kupamba | C. kukata | D. kuvunja |
| 15. | A. kutokomea | B. kulalama | C. kufululiza | D. kufumukana |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

16. Chagua jibu ambalo si sahihi
    A. Tai ni ndege mkubwa alaye mizoga.
    B. Chuma ni mtu mwenye nguvu.
    C. Kata ni eneo dogo la uwakilishani.
    D. Mbuzi ni kifaa cha kutengeneza chapati.
17. Nomino kutokana na kitenzi -la- ni
    A. kulala. B. chakula.
    C. kilio. D. kulaza.
18. Geuza sentensi hii katika usemi wa taarifa
    Mwalimu aliwambia wanafunzi,
    "Tutakamilisha funzo hili leo."
    A. Mwalimu aliwambia wanafunzi kuwa watakamilisha funzo hilo leo.
    B. Mwalimu aliwambia wanafunzi kuwa watakamilisha funzo hilo siku hiyo.
    C. Mwalimu aliwambia wanafunzi kuwa wangekamilisha funzo hilo siku hiyo.
    D. Mwalimu aliwambia wanafunzi kuwa angekamilisha funzo hilo siku hiyo.
19. Chagua sentensi iliyotumia kiigizi.
    A. Lo! Maria ameolewa akiwa mdogo hivyo?
    B. Mkifika mapema mtanipata papa hapa.
    C. Sarafina amekuwa kasuku wa kuyaiga ya wengine.
    D. Sote tulinyamaza ji mwalmu alipoingia darasani.
20. Ni pambo lipi kati ya haya huvaliwa masikioni?
    A. Kipuli. B. Pini.
    C. Hazama. D. Kipini.

21. Zote zilimbwa katika sherehe zote zilizofanywa jana. Tambua aina za maneno yaliyopigiwa kistari.
A. Nomino, kivumishi, nomino.
B. Nomino, kiwakilishi, kielezi.
C. Kiwakilishi, kivumishi, kielezi.
D. Kivumishi, kiwakilishi, kielezi.

22. Chagua sentensi yenye kitenzi -jina
A. Umati wa watu ulishuhudiwa sherehenî.
B. Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi.
C. Kutembea kwake kunawachosha wengi.
D. Simu ya Wambui ilipokinza hakuichukua.

23. Chagua sentensi yenye kielezi cha wakati
A. Tulipofika shuleni tuliingia darasani.
B. Walifanyizwa kazi kipunda wa dobi.
C. Mama huja shuleni mara kwa mara.
D. Nitasoma kwa bidii niwe daktari maishani.

24. Ni sentensi ipi yenye 'na' ya kuonyesha mtendaji?
A. Mgonjwa ana homa ya matumbo.
B. Daktari anawatibu wagonjwa vizuri.
C. Wakimbiaji watashindana kuwania ubingwa.
D. Mtoto atalishwa chakula na mjakazi.

25. **Kanusha:**
*Gari lililonunuliwa litauzwa tena.*
A. Gari lililonunuliwa halitatuzwa tena.
B. Gari ambalo halikununuliwa halitauzwa tena.
C. Gari lisilonunuliwa litauzwa ena.
D. Gari litakalonunuliwa litauzwa tena.

26. **Geuza sentensi hii katika umoja.**
*Vyakula vyote vimepikwa vikaiva*
A. Chakula zote zimepikwa zikaiva.
B. Chakula yote imepikwa ikaiva.
C. Chakula chote kimepikwa kikaiva.
D. Chakula lote limepikwa likaiva.

27. Ni orodha gani iliyo na viwakilishi vya nafsi pekee?
A. Mimi, sisi, wewe, nyinyi.
B. Wako, wenu, yangu, zao.
C. Huyu, kile, haya, humu.
D. Gani, lini, nini, gani.

28. Chagua sentensi iliyo sahihi kisarufi.
A. Humu ndimo walipoingia wezi.
B. Hapa sipo mlikoulizia.
C. Kule mlimoketi kuna siafu.
D. Amebeba mzigo kichwani pake.

29. Sentensi, "Nisingalimwona nisingalimpa ujumbe wake". Inamaanisha
A. nilimpa ujumbe ingawa sikumwona.
B. sikumpa ujumbe kwa kutomwona.
C. maadam nilimwona nilimpa ujumbe.
D. ujumbe ndio ulionifanya nimwone.

30. Kamilisha majina ya makundi yafuatayo.
Mwalimu mwenye _________ la nywele amevishwa ________ la maua.
A. koja, shada.
B. shungi, koja.
C. korija, koja.
D. chane, shungi.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Ili taifa kustawi na kuendelea kupiga hatua kimaendeleo, amani ni muhimu sana. Ili shughuli za mtu yeyote ziendeshwe vyema, sharti kuwepo na amani. Hivi ni kusema kuwa katika mazingira ya mwanadamu yeyote sharti yawe na amani na utulivu. Ni vyema kila mmoja wetu ajue kwamba ukosefu wa amani na utulivu, tuishipo, huzidisha ama kusababisha gharama kubwa ambayo kwa ***paruwanja*** haiwezi ikalipika kwa urahisi. Huu ndio wakati ambapo waja hupoteza mali yao ambayo huharibika na baya zaidi waja wengi wasio na habari kupoteza maisha yao. Aidha maendeleo katika maeneo yasiyo na amani hukwama. Isitoshe haki za wanadamu hukiukwa kwani wengi wa wahasiriwa hawapati mahitaji muhimu kama chakula, mavazi, elimu na nyingi nyinginezo.

Nchini zipo jamii zinazozozana kila uchao, nazo zimekuwa ni kielelezo cha uozo uliokita mizizi nchini. Zipo jamii ambazo hadi sasa zinashiriki wizi wa mifugo. Si lazima nizitaje jamii hizo ambazo zinashiriki uovu huo. Jamii hizo hulazimika kugura mara kwa mara kwa kuhofia kuwa huweza kuvamiwa na jamii hasimu. Kawaida ni kuwa hawawezi kuwa na makao ya kudumu kwani leo kesho huenda watahamia kusikojulikana.

Wanapohama, huacha mali yao na katika hali hiyo jamaa zao husambaratika. Jamii zinazoshiriki uovu huu huwa ni zile zinazopiga ubwete zisizotaka kuchoka. Wahusika huwa wazembe wa kujichumia mali yao. Huu ni uzembe wa hali ya juu. Ni nani asiyejua kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame? Hawajui kuwa ngao ya kuazima haisitiri matako; ashakum si matusi?

Jambo jingine linalosababisha ukosefu wa amani ni ukosefu wa ajira kwa vijana. Vijana hawa wanapokosa cha kujikimu husawishika kuingilia vitendo hasi mfano wa wizi wa mabavu na ukahaba. Aidha vijana wawa hawa kwa shinikizo la rika huanza kuuza na kutumia dawa za kulevya na kushiriki ujangili. Zaidi ya yote, vijana wawa hawa ndio wanaotumiwa visivyo na wanasiasa kutekeleza uhalifu na matakwa yao. Kupitia mikutano hiyo, wanasiasa hupata fursa ya kupalilia uhasama wa kikabila na kimaeneo. Vijana hao hao mara nyingi kwa kutotumia akili zao huvamia na kuharibu mali.

Ili kukabiliana na hali hii ya ukosefu wa amani, washikadau wote wanastahili kuchanga bia. Jamii na wananchi wanapaswa kuelezwa kuhusu umuhimu wa amani. Jamii zinazojihusisha na maovu kama vile wizi wa mifugo zinapaswa

kuhamasishwa na kusaidiwa kwa namna moja au nyingine kujikimu kwa juhudi zao wenyewe. Serikali nayo ni sharti ijumuike kwa kuvunda viwanda na kampuni nyingi ili vijana waliohitimu masomo wapate ajira. Vilevile serikali yetu ni bora itenge fedha kiasi za kuwapa vijana kuanzisha biashara ndogondogo kwa lengo la kujikimu na kujiendeleza. Iwapo haya yatafanyika, basi hatuna budi kiushi katika jamii yenye amani na hivyo uchumi wa taifa letu utaimarika.

31. Kulingana na aya ya kwanza, ni sahihi kusema kuwa
   A. watu huendesha shughuli zao kama kawa bila kuzingatia sana amani.
   B. kukosekana kwa amani huweza kuimarisha maendeleo ya nchi.
   C. gharama ya maisha na hasara hutokea sana pasipo na amani.
   D. wapigao ndio hasa hukosa mahitaji muhimu huku wasio na hatia wakiishi vizuri.

32. Neno paruwanja limetumiwa katika ufahamu. Lina maana gani?
   A. Uhasama.
   B. Bila kuficha.
   C. Bile taabu.
   D. Kwa hali na mali.

33. Haki za binadamu zilizotajwa katika ufahamu si pamoja na
   A. maendeleo.
   B. chakula.
   C. makazi.
   D. elimu.

34. Ni maovu gani yanayotajwa ufahamuni kuwa ya jadi na yaliyopitwa na wakati?
   A. Ujangili.
   B. Wizi wa mabavu.
   C. Utumizi wa dawa za kulevya.
   D. Wizi wa mifugo.

35. Ni dhahiri kwamba jamii zinazoshiriki uovu wa kuwaibia wengine ni wale
   A. wasiothamini maendeleo.
   B. wanaopenda udugu.
   C. wapigao ubwete.
   D. wachapakazi na wazalendo.

36. Mtu asiyetoa jasho bali hutegemea jasho la wengine huweza kusutwa kwa methali
   A. upweke ni uvundo.
   B. heri jirani wa karibu kuliko ndugu wa mbali.
   C. mchagua jembe si mkulima.
   D. mtembezi hula miguu yake.

37. Maswali yaliyoulizwa katika aya ya tatu ni yale yasiyohitaji majibu. Huitwa maswali ya
   A. balagha.
   B. methali.
   C. misemo.
   D. hekima.

38. Ukosefu wa ajira za vijana umesababishaje ukosefu wa amani nchini?
   A. Vijana wengi hushiriki siasa.
   B. Vijana hujiajiri kwa mikopo ya serikali.
   C. Vijana hushiriki vitendo viovu.
   D. Vijana hujitahidi na kujikomboa.

39. Katika mikutano ya kisiasa, wanasiasa
   A. hupalilia uadui wa kikabila na wa kimaeneo.
   B. huwachochea vijana kujiunga katika vikundi na kupata mikopo ya serikali.
   C. huwahamasisha vijana kujiajiri.
   D. huwapa vijana fedha za serikali kuanzisha biashara ndogondogo.

40. Ni gani si mojawapo ya suluhisho zinazopendekezwa na mwandishi katika aya ya mwisho?
   A. Kuanzisha miradi ya kuwaelimisha vijana.
   B. Kujenga kampuni ili kubuni nafasi za ajira.
   C. Kutega fedha kiasi cha haja za kuwakopesha vijana kuanzisha biashara.
   D. Jamii na wananchi kwa jumla kupata hazisho kuhusu umuhimu wa amani.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.</u>***

Baada ya kumaliza hamsini zangu tele zisizo na kikomo mchana kutwa, jioni hiyo kama desturi nilikuwa na uchovu wa punda wa dobi. Daima ***<u>nilijitoa sabili</u>***, kufa kupona kama wanaume wenzangu wa Bondamali ili kuifaa aila yangu. Niliazimia kuanzisha aidha kampuni ya maziwa ama nipanue ufugaji wa ng'ombe wa nyami-almaarufu, maksai. Bora kuyaboresha maisha; madhali, kazi ni kanzi, niliipa akiba kipaumbele kwani haiozi.

Kwa hivyo, nilikuwa nimeibwa na gonezi mnamo mida ya saa nne-ghafla niliposhtuliwa na mguso wa ahali wangu. "Amka! Nasikia ***<u>nyende</u>*** sijui ni za nini!" Akanisihi. Mwanzo nilijitia hamnazo kwani tulizoea kelele za wapiga mtindi waliobugia chupa za vileo na vizibo vyao. Kitalifa kidogo kutoka kwetu palikuwa na klabu kilichouza mtindi haramu na halali. Halafu aliwasha kibatari na kukaa ange kama sungura aliyehisi hatari.

Mie nilijaribu kulala ila nikajiwa na usingizi wa mang'amumang'amu kwani nafsi yangu ilikuwa na atiati. Ghafla kama ajali mwangwi mzito ukasikika dhahiri, "Wezi! Wezi! Saidieni!" Lo! ilikuwa sauti ya mama Subira mjane aliyefiwa karibu miezi minne iliyopita. Aliachwa mfaruku wa mabinti wanne kasoro mvuli. Huenda wengi walimlilia ngoa kwa shamba kubwa aliloachiwa ilhali hakujaliwa mtoto wa kiume. Mila potovu zilimnyima mwanamke uwezo wa kumiliki mali.

Kwa muda wa bana banua, sikujua la kufanya wala kusema. Wakati huo watoto walikuwa macho chumbani mwao wakikohoakohoa kwa hofu. Ahali wangu naye alibaki tisti kama sanamu huku mdomo ukiwa achama; falau pango. Mie sikudiriki kufanya ajizi. Nilinyatanyata kwa ujasiri hadi mlangoni kisha nikaufungua. Mkononi, nilijihami kwa kurunzi kubwa iliyomlika mwanga wa jua na sime kali iliyonolewa ikapata. Nilijiegemeza mlangoni kwa tahadhari kuu mithili ya ***tabibu mpasuaji***.

Niliposikia michakacho kadhaa huko nje, kweusi tititi na tulivu kama kaburi, niliamua kumulika kurunzi. Kwa sadfa, mionzi ililiangaza janadume lililojarbu kujibanza kichakani. Jibwa langu lilibweka kwa takizi likaamka na kutifua ghubari kulikabili jizi hilo. Kwa mwia wa kufumba na kufumbua; wanaume wachache walijitoma gizani kunipa mkono kulisaka jizi hilo lililovizia mali ya wenyewe. Wengine walifunga malango yao ya njia za pembeni ili pasiwe na upenyo wowote.

Wanaume walishirikiana zaidi ya kufuli na ufunguo kulisaka kwa jina na ukucha. Aisee! Za mwizi ni arubaini tu. Jibwa langu lililifumania katika magomba nyumbani pa Mzee Salama. Mapigo ya kitutu yakatamalaki. Sikuambii marungu, mateke, makofi na hata magogo vilishirikiana kulipa adhabu ya mwaka. Jambazi hilo hatimaye likafikishwa kituoni pa polisi. Nasi tukakubaliana kudumisha amani na usalama kwa hali na mali.

---

**41.** Kwa mujibu wa aya ya kwanza

A. mwandishi alikuwa mwalimu wa Bondamali.

B. mwandishi alikuwa mfugaji wa ng'ombe dume awali.

C. mwandishi alilala kabla ya wakati.

D. aliazimia kuweka akiba baadaye maishani.

**42.** Ni nini maana ya "nilijitoa sabili"?

A. Kutekeleza majukumu.

B. Kufahamu siri iliyofichwa na kufichua.

C. Kutoa msaada kidogo.

D. Kujitolea mhanga.

**43.** Mbali na tochi, mwandishi alikuwa na zana ipi ya vita?

A. Mkuki.

B. Ngao.

C. Mishale.

D. Sime.

**44.** Kwa mujibu wa makala haya, ni kweli kuwa

A. wanajamii walizingatia haki kwa jinsia zote.

B. yaelekea mwizi alipanga kuiba shamba lile la mjane.

C. mwandishi alikuwa jasiri na mtetesi wa wanyonge.

D. baadhi ya walevi walipiga kelele nyingi siku hiyo.

**45.** Punde mwandishi alipoamshwa

A. alipuuza kwa kudhani kuwa zilikuwa ni kelele za walevi.

B. alinyatanyata kwa woga hadi mlangoni.

C. aliwaamsha watoto pia.

D. alishikwa na usingizi wa pono.

**46.** Tochi ilimulikwa wakati gani?

A. Mbwa alipobweka.

B. Baada ya kusikia michakacho.

C. Kulipokuwa kweusi nje.

D. Jizi lilipojibanza.

**47.** Kulingana na aya ya mwisho; ni kweli kusema

A. walioshirikiana kumsaka mwizi walikuwa wanaume.

B. wanawake nao walibeba zana za vita.

C. mwizi alipatikana na mbwa akiwa kichakani katika msitu.

D. mwizi alimpiga mbwa akafa.

**48.** Mapigo ya kitutu ni yapi?

A. Kupigwa kwa silaha butu.

B. Kupigwa bila huruma.

C. Kupigwa na watu wengi.

D. Kupigwa na kuumizwa vibaya.

**49.** Neno ahali limetumika, likiwa na maana gani?

A. Mzuwanda.

B. Mke.

C. Mkwe.

D. Mnuna.

**50.** Methali inayoelezea ushirikiano wa wanakijiji ni gani?

A. Siku za mwizi ni arubaini.

B. Chema hakidumu.

C. Mnyonge hana haki.

D. Jifya moja haliinjiki chungu.